**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**
**MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA SITA**

**121/1**

# KISWAHILI 1

(Kwa Watahiniwa Walioko Shuleni na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda: Saa 3** **Jumanne, 08 Mei 2018 asubuhi**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E zenye jumla ya maswali **kumi (10)**.
2. Jibu maswali **saba (7)** kwa kuzingatia maelekezo kutoka katika kila sehemu.
3. Kila sehemu ina alama **ishirini (20)**.
4. Simu za mkononi, vikokotozi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



ACSEE-0518

Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

## SEHEMU A (alama 20)
## UFAHAMU

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Soma kwa umakini kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu kwa usahihi maswali yanayofuata.

Kipindi cha kuanzia mwaka 1930 hadi 1938 kilikuwa muhimu sana kwa historia ya **usanifishaji** wa Kiswahili. Mambo mbalimbali yalifanyika ili kuhakikisha kuwa Kiswahili kinastawi na kushamiri. Kuundwa kwa kamati maalum ya kushughulikia lugha ya Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki, ilikuwa hatua muhimu sana katika kukikuza na kukieneza Kiswahili.

Kazi za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki zilikuwa nyingi kama vile, kusanifisha otografia itakayotumika kwa watumiaji wote wa Kiswahili, kuandaa kamusi mbalimbali, kutoa hamasa kwa waandishi wachanga wanaotumia lugha ya Kiswahili katika kuandika kazi zao, kusahihisha lugha katika vitabu vilivyokuwa vinatumika kufundishia shuleni na kufanya tafiti mbalimbali za lugha ya Kiswahili.

Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki ilifanya kazi chini ya usimamizi wa utawala wa mwingereza. Kazi za kamati **zilipamba moto** huku tafiti mbalimbali kuhusu **lahaja** za Kiswahili zikiendelea kufanyika. Tafiti hizo zilizaa matunda na hatimaye ikaonekana ni vizuri kuchagua lahaja moja na kuisanifisha ili iwe msingi wa **Kiswahili sanifu**.

"Mungu hamtupi mja wake," **sudi** iliangukia kwa lahaja ya kiunguja na ilichaguliwa kuwa lahaja ya Kiswahili sanifu. Watumiaji wa lahaja zingine walikuwa na inda baada ya lahaja ya kiunguja kutangazwa kuwa msingi wa usanifishaji wa Kiswahili. Kamati haikufanya ajizi, ilianza mara moja kusanifisha lugha ya Kiswahili. Kiswahili sanifu tukitumiacho leo ni matunda ya kazi ya utawala wa mwingereza katika usanifishaji wa lahaja ya kiunguja.

Kwa ujumla tunaweza kusema kati ya wakoloni wote, wakoloni wa Kiingereza ndio waliofanya kazi kubwa katika kuikuza na kuiendeleza lugha ya Kiswahili. Kupitia sera na mfumo wa utawala wa wakati huo walifanya kazi kubwa kuhakikisha kuwa Kiswahili kinakua na kuenea katika nchi za Afrika Mashariki.

**Maswali**

(a) Andika kichwa cha habari hii kwa maneno matatu.

(b) Toa maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika habari uliyoisoma.

(i) Usanifishaji

(ii) Zilipamba moto

(iii) Lahaja

(iv) Kiswahili sanifu

(v) Sudi



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

(c) Usemi "Mungu hamtupi mja wake," una maana gani?

(d) Mwandishi anauelezeaje mchango wa wakoloni wa Kiingereza katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili?

2. Fupisha habari uliyoisoma kwa maneno **mia moja**.

**SEHEMU B (Alama 20)**
**MATUMIZI YA SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA**
Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

3. Fafanua maana ya dhana za sarufi ya Kiswahili zifuatazo:
   (a) Ngeli za majina
   (b) Mofimu
   (c) Kirai
   (d) Sentensi
   (e) Mzizi

4. Kwa kutumia mifano kutoka katika lugha ya Kiswahili, toa hoja tano kubainisha tofauti kati ya mofimu tegemezi na silabi.

5. Kwa nini ni muhimu kuzingatia uhusiano baina ya wahusika wakati wa kutumia lugha? Toa hoja tano.

6. Toa maana tano za neno pasi na kwa kila maana tunga sentensi moja.

**SEHEMU C (Alama 20)**
**UTUNGAJI**
Jibu swali la **saba (7)**.

7. Jifanye wewe ni Afisa Habari wa Shirika la Ndege Tanzania, andika tangazo kwa abiria kuhusu katizo la usafiri wa ndege NAMBA TY JET 343 iliyokuwa ifanye safari yake toka Songea kwenda Zanzibar siku ya Ijumaa tarehe 25/5/2018 saa 12 asubuhi, kuwa safari hiyo itafanyika Jumapili tarehe 27/05/2018 saa 8 mchana. Mabadiliko haya yanatokana na kuchafuka kwa hali ya hewa angani. Jina la mtoa tangazo liwe **Kudura Riziki**.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

## SEHEMU D (Alama 20)
## MAENDELEO YA KISWAHILI

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

8. Jadili changamoto sita zinazoikabili lugha ya Kiswahili nchini Tanzania.

9. Fafanua sababu sita zilizochangia lugha ya Kiswahili isikue na kuenea kwa kiwango kikubwa nchini Uganda kabla ya uhuru.

## SEHEMU E (Alama 20)
## TAFSIRI NA UKALIMANI

Jibu swali la **kumi (10)**.

10. Katika Tanzania ya leo taaluma ya tafsiri haiwezi kuepukika. Kwa kutumia hoja tano, thibitisha kauli hiyo.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

Scanned by CamScanner